

**TAMKO LA MHE: MKUU WA MKOA WA PWANI WAKATI WA UZINDUZI
WA KAMPENI YA UTOAJI WA CHANJO YA KUZUIA UGONJWA WA
POLIO KWA WATOTO CHINI YA MIAKA MITANO**

TAREHE 18 MEI, 2022

UKUMBI: OFISI YA MKUU WA MKOA

Ndugu Wanahabari,

- Nimewaita hapa kuwapa taarifa ya chanjo ya Polio kwa Watoto chini ya miaka mitano. Kampeni hii inatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe **18 Mei-21 Mei, 2022** ndani ya mkoa wetu.

Ndugu wanahabari,

- Mnamo tarehe 17 Februari, 2022 Serikali ya Malawi ilitoa tamko la kuwepo kwa mlipuko wa ugonjwa wa polio katika nchi hiyo baada ya mtoto mmoja kutoka nchi hiyo kuthibitika kuwa na ugonjwa katika mji mkuu wa Nchi hiyo; Lilongwe. Hii inakuwa ni mara ya kwanza kwa bara la Afrika kutokea kisa hicho baada ya kupita miaka mitano bila kisa cha ugonjwa huo.

Ndugu wanahabari,

- Baada ya kupata taarifa za uwepo wa mgonjwa nchini Malawi, Serikali kupitia Wizara ya Afya inapenda kuwajulisha wananchi kuwa kutakuwa na kampeni ya utoaji wa chanjo ya kuzuia ugonjwa wa Polio nchini kote. Kampeni hii itafanyika kuanzia tarehe 18 Mei hadi 21 Mei 2022 na itahusisha kutembelea nyumba kwa nyumba na kutoa chanjo kwa walengwa, ambao ni watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano.

Ndugu wanahabari,

- Madhara makubwa ya ugonjwa wa polio ni ulemavu wa ghafla wa viungo, hivyo sambamba na kampeni hii; shughuli za ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za wagonjwa wote wanaopata ulemavu wa ghafla zitafanyika. Ugonjwa huu huathiri zaidi watoto chini ya miaka 15 hivyo ufuatiliaji wa watoto wa umri huo wanaopata ulemavu wa ghafla utaimarishwa ili wapatiwe matibabu stahiki.

Ndugu wanahabari,

- Ili kupata kinga kamili dhidi ya ugonjwa wa Polio, chanjo hutolewa kwa dozi 4 ambapo dozi ya kwanza hutolewa mtoto anapozaliwa, ya pili anapofikisha umri wa wiki 6, ya tatu wiki 10 na ya nne wiki 14. Ni muhimu mtoto akamilishe ratiba ya chanjo kama inavyotakiwa ili apate kinga kamili.

Ndugu wanahabari,

- Kampeni hii inalenga kutoa chanjo kwa jumla ya watoto 200,967 katika Mkoa wetu. Aidha, watoto wote chini wa miaka mitano watapata chanjo hii bila kujali kama walishapata chanjo hii katika ratiba zao za kawaida za chanjo. Wazazi wenye watoto ambao hawajapata kabisa chanjo na ambao hawakukamilisha ratiba ya chanjo wanasisitizwa kuwepo majumbani tarehe hizo. Na endapo tarehe za kampeni zitapita pasipo kufikiwa na huduma hii, basi wanaombwa wafike kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vilivyo karibu ili kupata chanjo.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA